# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

**Telegramu:"LEGAL"**
**Simu Na.:** +255 26 2310019
**Nukushi:** +255 26 2310056
**Barua Pepe:** km@sheria.go.tz
**DodomaTovuti:**www.sheria.go.tz

Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Katiba,
S. L. P. 315,
**40484 DODOMA**

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## MAFANIKIO YA KIKAO CHA 77 CHA KAMISHENI YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU KILICHOFANYIKA JIJINI ARUSHA 20 OKT – 09 NOV 2023.

**Arusha, 11 Novemba, 2023.**

Tanzania imekuwa mwenyeji wa Kikao cha 77 cha Kawaida cha Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kilichofanyika kuanzia tarehe 20 Oktoba hadi 9 Novemba, 2023 katika ukumbi wa kimataifa wa mikutano wa Arusha (AICC) Jijini Arusha. Kikao hiki kimefanyika kwa mara ya kwanza katika ardhi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na vilevile kwa mara ya kwanza ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kikao kilifunguliwa rasmi tarehe 20 Oktoba 2023 na ***Mhe. Dkt. Hussein Ally Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi*** kwa niaba ya **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**. Jumla ya wageni na wajumbe wapatao 1,860 kutoka mataifa wanachama na mataifa waangalizi wameshiriki Kikao hiki. Mbali na Tanzania Mataifa mengine ni Algeria, Angola, Afrika Kusini, Benin, Botswana, Burundi, Burkina Faso, Cape Verde, Chad, Cameroon, DR Congo, Ethiopia, Equatorial-Guinea, Eritrea, e-Swatini, Gambia, Guinea -Bissau, Ghana, Ivory Coast, Kenya, Liberia, Libya, Lesotho, Madagascar, Malawi, Mauritania, Mali, Misri, Morocco, Msumbiji, Nigeria, Niger, Rwanda, Senegal, Somalia, Sudan, Togo, Tunisia, Uganda, Zambia na Zimbabwe ambapo yaliwasilisha taarifa za hali ya Haki za Binadamu katika nchi zao. Aidha, Nchi waangalizi zilizohudhuria Kikao hiki ni pamoja na Denmark, Marekani, Ubelgiji, Uingereza, Ufaransa, India, Paraguai pamoja na Uswisi.

Tanzania, kupitia Waziri wa Katiba na Sheria iliwasilisha taarifa ya hali ya Haki za Binadamu na Watu nchini ikionesha jinsi Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inavyotekeleza na kusimamia haki za binadamu kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yam waka 1977, Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo. Aidha taarifa hiyo ilibainisha haki za binadamu zimeainishwa katika katiba kuanzia Ibara ya 12 hadi 24 na pia Ibara ya 25 hadi 30 zinayoainisha wajibu wa kila raia. Katika kuhakikisha haki za binadamu na watu zinalindwa, Serikali ilianzisha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ambacho ni chombo cha Kikatiba kinachoshughulikia masula ya Haki za Binadamu ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kutetea, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu nchini.

Wajumbe waliipongeza Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukuza na kulinda haki za binadamu na watu ikiwa ni pamoja na kuzingatia mahitaji wa watu wenye mahitaji maalum ambapo tarehe 21 Oktoba, 2023 Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipewa tuzo na Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na watu.

Mathalani, Mwenyekiti wa Kamisheni aliipongeza Tanzania kwa kuweka Wakalimani wa lugha ya alama kipindi chote cha Kikao kuhakikisha watu wenye ulemavu wa usikivu (viziwi) wanapata fursa ya kufuatilia Kikao hiki.

Kwa kuwa mwenyeji wa Kikao hiki, Tanzania imepata Mafanikio ya Kijamii na Kiuchumi. Miongoni mwa mafanikio hayo ni: -

i. Matumizi ya Lugha yetu ya Kiswahili katika siku zote za Kikao pamoja na kuweka Wakalimani wa Kiswahili;

ii. Kwa mujibu wa Taarifa ya Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha AICC-Arusha, takribani Shilingi Bilioni 18 zimeingia kwenye mzunguko na hivyo kuleta matokeo chanya katika uchumi wa Mkoa wa Arusha na Taifa kwa jumla ambapo jumla ya Watoa huduma za Malazi wapato 123, wajasiliamali wadogo wadogo katika tasnia ya mavazi na urembo zaidi ya 100, watoa huduma za vyakula wapatao 100, watoa huduma za usafiri wa barabara zaidi ya 100, watoa huduma za vifaa vya mikutano wa tano (5) na vikundi vya Sanaa vitano (5) wamenufaika moja kwa moja. Vilevile, jumla ya wageni 870 wametembelea vivutio vya utalii vilivyopo mkoa wa Arusha;

iii. Kuimarika kwa mahusiano ya kimataifa baina ya Tanzania na Nchi za Umoja wa Afrika, Mashirika ya Kimataifa, Jumuiya za Kikanda na Kimataifa, Asasi za Kiraia na Mashirika yasiyo ya Kiserikali na Washirika wa Maendeleo katika tasnia ya haki za binadamu na sheria katika kukuza na kulinda haki za binadamu na haki za watu. Mhe Balozi Pindi Chana, Waziri wa Katiba na Sheria alikutana na Mawaziri wote waliofika, Mabalozi wa nchi pamoa na Viongozi kutoka mashirika na Taasisi mbalimbali za haki za binadamu wakiwemo Mwenyekiti wa Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Rais wa Mahakama ya ECOWAS, Baraza la Umoja wa Mataifa wa Haki za Binadamu (UN Human Rights Council) na Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Binadamu (Office of the UN High Commissioner for Human Rights).

iv. Kupitia kikao hiki, Tanzania imeidhihirishia Afrika na dunia kwa ujumla uwezo ilionao katika kupokea na kuwahudumia wageni wengi na kuwahakikishia usalama wao kwa muda wote ambao wamekuwa katika nchi yetu ambapo jumla ya wageni 1,870 wamehudhuria kikao hicho Jijini Arusha.

Wizara inamshukuru Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, kwa uamuzi wake wa kuridhia na kuwezesha kikao hiki kufanyika nchini Tanzania. Vilevile, Waziri anawashukuru Wajumbe wa Sekretarieti ya Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na kamati ya kitaifa ya hapa nchini iliyoandaa kikao hiki kwa kazi kubwa waliyofanya na kufanikisha kikao hiki muhimu kwa Taifa. Aidha, Mhe. Waziri anawashukuru sana Wananchi wa Jiji la Arusha kwa ushiriki wao pamoja na Wanahabari kwa kushiriki na kuuhabarisha umma kuhusu Kikao hiki.

***Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Ibariki Afrika.***
***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.....Kazi iendeleee***

**Lusajo Mwakabuku**

**MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**